



**TASAF KICHOCHEO CHA MAENDELEO KARAGWE.**

Mradi wa TASAF umekuwa kichocheo kikubwa cha maendeleo kiasi kwamba baadhi ya familia zilizokuwa na mazingira magumu zimefikia hatua ya kujenga nyumba za kudumu kwa kutumia ruzuku inayopokelewa kutoka mradi huo.

Wahitaji/Walengwa kwa nyakati tofauti wamefikia kulimbikiza ruzuku inayokusanywa kutoka TASAF na kuanzisha miradi midogo midogo tofauti hatimaye wakifikia malengo ya kujenga nyumba za tofari, japokuwa ziko katika level tofauti kumalizia kulingana wakati wa kujiunga na utashi.

Bi Thelezia Gosbert Kiiza kutokea Kijiji cha Kanoni kwenye Kata ya Kanoni amefikia hatua hiyo ya kujenga nyumba ya kudumu, baada ya kuchukuwa malimbikizo ya ruzuku kutoka TASAF na kununua Mashamba hatimaye kwenye msimu wa mavuno huuza magunia ya maharage yasiyopungua matatu hadi matano kisha kununua vifaa vya ujenzi.

‘‘Baada ya kupata ruzuku ya TASAF nilianza kununua shamba, baada ya hapo nikaanza kulima, hapo hapo nachanganya mavuno kutoka shambani na ruzuku ninayopokea kila baada ya miezi miwili mwisho wa siku mnaona nyumba ilipofikia, tayari nina mbuzi watatu majike’’ alisema Bi. Thelezia Gosbert.

Ukweli Mradi wa TASAF una umuhimu mkubwa kwani kwa kipindi cha nyuma hasa wakati wa baa la njaa tulikuwa tumefika kula mlo mmoja kwa siku alisema.

Kwa hivi sasa watu tuna uhakika wa kula milo mitatu bila wasiwasi na baada ya kuwa na uhakika mzuri wa kula ndipo tunapofikiria kujenga nyumba na kufanya maendeleo mengie kama kujenga visima vya maji kwani Kata yetu ina tatizo la maji.

Bi. Thelezia amesema kipindi cha nyuma ilifikia hatua wanafunzi walishindwa kwenda shule wanaishia kwenda kufanya kazi za vibarua kwa watu ili wapate unifomu na ada ya shule lakini kwa sasa mahudhuria yao shuleni ni mazuri sana.

Kwa muda huu naona hata wanafunzi wanaofaulu mtihani wa darasa la saba kwenda kidato cha kwanza, sisi wazazi hatuhangaiki kwenda kukopa kwa watu au watu wengine waliokuwa na mashamba ya ulithi kufukilia kuyauza ili mtoto aende shule.



**MABIBI KIZEE WAWILI WAJIFUNZA UJASILIA MALI BAADA YA KUWEZESHWA NA TASAF**

Mradi wa TASAF wachangamusha akiri ya watu katika Kijiji cha Kibona katika Kata ya Kanoni hadi kufikia hatua ya mabibi kizee wawili kujifunza ujasilia mali mmojawapo akianzisha mradi wa mama ntilie huku mwingine akianzisha kibanda cha matumizi madogo madogo ya nyumbani.

Akiongea na mwandishi wa habari hii Bi. Rusia Nyangoma Kashaija mwenye umri wa miaka 62, amesema akitokea kwenye dirisha la malipo, alipanga kuanziasha mgahawa ili umsaidia kuwa anapata riziki ya kila siku ambayo jumla kwa mwezi anapata zaidi ya elfu sitini.

Aidha, naye Bi. Reveth Bairi Rafaely mwenye umri wa miaka 68 alianzisha Mradi wa Kibanda cha duka ambacho anauza sabuni, madaftari , soda na vifaa vingine vya madukani vya matumizi ya kawaida na kwa mwezi anapata wastani wa Tzs. 40,000/= kama faida.

Wakiongea kwa nyakati tofauti wamesema kila wakipata ruzuku yao kila baada ya miezi miwili hupanga jinsi ya kuongeza kwenye mitaji yao na nyingine hutumia kwenye matumizi yao ya kawaida kama kununua chakula kulipia ada ya wanafunzi na matumizi mengine ya kawaida.

Pamoja mitaji yao kuwa midogo tayari watu hao wameisha rekebisha nyumba zao za kuishi , mfano Bi. Rusia Nyangoma Kashaija nyumba yake ilikuwa finyu yenye bati tisa, sasa baada ya upanuzi imefikia bati kumi na nne ambayo inawatosha kifamilia.

Naye Bi. Reveth Bairi Rafaely tayari pamoja na upanuzi wa nyumba tayari ameisha nunua mbuzi watatu , kuku nne nguruwe 1 na bata 1 hivyo anasema bado anaendelea na kuongeza idadi ya mifugo.

Bi. Rusia yeye anasema anampango wa kuanza kufuga nguruwe kwa maana kwenye mgahawa wake ana mwanga vyakula vinavyobaki baada ya kuuza kwa siku, hivyo akiwa na nguruwe hata patashida ya kumrisha, ambayo ni tofauti na mbuzi ambao anabidi kuwapeleka kwenye marisho wakati muda wake mwingi anakuwa kwenye mgahawa.





**MBUZI ,NGURUWE, KUKUNA SUNGURA NI MIFUGO INAYOLETA TIJA KWA HARAKA**

Imesemekana kuwa aina ya mifugo kama Mbuzi, Nguruwe, Kuku na sungura huleta faida na tija kwa kipindi kifupi na gharama ndogo kwa mfugaji ikiwa ni ya kawaida haimsumbui.

Hayo yamesemwa na baadhi ya walengwa wa mradi wa TASAF katika Kijiji cha Runyaga, Kata ya Chanika Wilayani Karagwe, ambapo wamesema kwa mwaka mbuzi huzaa mara mbili , nguruwe huzaa mara mbili na vitoto vingi vya kutosha huku kuku huzaa hata mara tatu na vifaranga vya kutosha.

Aidha, imeelezwa hata ufugaji wake hausumbui mfugaji kwani kwa nguruwe hasumbui na uzuri wake habagui chakula na mbuzi hivyo hivyo hufunguliwa muda fulani kupelekwa polini labda la msingi ni kukumbuka kumuogesha na saa nyingine kumjali dawa za minyoo wakati kuku ikiwa ni kipindi baada ya mavuno ya msimu huachiwa wanajitafutia chakula wenyewe.

`` Ukweli ni kwamba kwa upande wangu naona mbuzi vyepesi kufugika kwani mbuzi akila majani yenye unyevunyevu humletea magonjwa ya midomo hivyo nasubiri wanafunzi wakitoka shule wnapeleka marishoni jioni hivyo hivyo kwa nguruwe ambaye hupewa hata mabaki ya chakula kilicho washinda ndani kwani yeye habagui aina yoyote ya chakula alisema Imelta Kokuteta Leopord.

Pamoja na ufugaji huo usiosumbua mfugaji aina ya mifugo tajwa hapo juu ukiamua mfano kama kuku unaanzia kwenye kuuza mayai na hata ukiamua atotoe vifaranga baada ya muda Fulani unaanza kuuza wale vifaranga hivyo huwezi kulia shida ndogo ndogo.

Kwa hivi sasa Karagwe yetu bei ya nguruwe hata kama ni mdogo haiwezi kupungu elfu 50,000/= na kwa uzao wa kawaida nguruwe mmoja huweza kuzaa kuanzia vitoto 8 hadi zaidi ya 14 hivyo ukiwatunza vizuri faida ina kuwepo, ile hali hata kwa mbuzi.

‘‘Kutokana na ruzuku ya TASAF tunayoipata kila baada ya miezi miwili ukijibana kila kitu kinawezekana kwani hadi sasa nimejenga nyumba kwa kutumia mradi hii midogo midogo’’alisema Imelta.